SALA YA ASUBUI
na *SALA YA JIONI*

MAFUNDISHO

Waisraeli wa zamani walikuwa na desturi ya kuabudu Mungu kila siku, asubui na jioni. Wengine waliomba vilevile kwa saa sita au saa tisa. Zaidi ya watu waliomba nyumbani, lakini wengine waliweza kukutana sunagogini‡.

Tunajua kwamba kila siku walisema, sawa sisi tunasema imani, mashairi haya: Kumbukumbu 6:4-9, 11:13-21, na Hesabu 15:37-41. Nyuma ya haya, kulikuwa maombi mbalimbali. Siku ya Sabato, pa sunagogi, walisoma vipande viwili, moja toka vitabu vya Sheria, na moja toka Wanabii. Watu wengi walijua Zaburi kwa kichwa, nao waliziimba katika ibada hekaluni, sunagogini na nyumbani.

Wakristo wa kwanza walidumu katika desturi ya wayuda, na hata wakati walifukuzwa toka hekalu na masunagogi, waliweza kuendelea na desturi zile katika ibada yao.

Katika karne ya ine nyuma ya Kristo, mutawala Konstantin wa Roma aligeuka kwa Kristo, na kulianza kuwa rahisi zaidi kwa wakristo kukutana kuabudu Mungu, hata kila siku. Askofu au kasisi aliongoza wakristo katika zaburi, nyimbo, na maombi.

Katika nyumba za watawa (*frères* na *soeurs*) kulikuwa desturi ya kuabudu pamoja mara tano au mara sita kila siku, wakisoma zaburi na vipande vya Maandiko Matakatifu. Kila shirika la watawa lilitengeneza taratibu yake ya sala za kila siku.

Katika Kitabu chake cha Sala cha 1549, Askofu Cranmer alichanga pamoja sehemu za taratibu za watawa, akifanya taratibu mbili tu. Kusudi lake lilikuwa wakristo *wote* wakutane mara mbili kila siku kuomba; lakini watu wachache waliweza.

Siku hizi Sala ya Asubui na Sala ya Jioni zinatumiwa zaidi kwa Siku ya Mungu (Siku ya Mungu); lakini katika makanisa na mashule mengine zinatumiwa kwa siku nyingine. Na watu wengine wanafurahi kuzitumia nyumbani, ili maombi yao ya jamaa au ya upekee yajae na maneno ya Biblia.

MAAGIZO

A MUHUDUMU ajifunze mbele ya wakati namna atapanga ibada. Kwa ibada isiyo ibada kuu ya Siku ya Mungu, anaweza kuchagua kusoma kipande kimoja tu. Kwa kawaida kipande hiki kiwe cha Agano Jipya, lakini kwa wakati wa Kuja kiwe cha Agano la Kale.

B NYIMBO ZA BIBLIA zinachapwa kwa kurasa 18-28. Kila moja inaweza kutumiwa kwa wakati wo wote, lakini kusaidia muhudumu kuna mashauri kwa n° 5 na n° 12 juu ya nyimbo zinazofaa kwa nyakati na siku mbalimbali.

C MATANGAZO yanaweza kutangazwa au nyuma ya vipande, au mwishoni mwa ibada.

D SALA YA KUKIRI ZAMBI: ile ya asubui inaweza kutumiwa jioni, na ile ya jioni inaweza kutumiwa asubui.

E MAOMBI YA KANISA: yale ya ibada nyingine yanaweza kutumiwa.

SALA YA ASUBUI

1† *Wakati wahudumu wanaingia, wote wasimame.*
Shairi la siku lisomwe.

2† *WIMBO uimbwe.*

3† *Muhudumu aseme:*
Tumekusanyika pamoja kama jamaa ya Mungu
mbele ya Baba yetu,
tukivutwa na Roho yake,
kusifu Jina lake,
kusikia na kupokea Neno lake takatifu.
kumwomba usamehe kwa zambi zetu,
kuombea mahitaji yetu na ya dunia,
kufurahi katika mapendo yake,
na kutumwa katika salama yake.

4 *Muhudumu* Ee Bwana, ufungue midomo yetu
Wote **Na kinywa chetu kitaonyesha sifa yako**

4a *Katika KUJA na KUFUNGA:*
Muhudumu Tumaini letu ni katika jina la Bwana
Wote **Aliyeumba mbingu na dunia.**
Muhudumu Ee Mungu, utuokoe kwa haraka.
Wote **Ee Bwana wetu, utusaidie kwa haraka.**

4b *Katika KUZALIWA, ONYESHO NA PASAKA:*
Muhudumu Matendo ya Bwana ni makubwa na ya ajabu!
Wote **Wakati tulikuwa tungali katika giza,**
alisikia kilio chetu.
Muhudumu Mapendo ya Mungu yameonekana kwetu.
Wote **Alituma Mwana wake,**
ili tupate uzima wa milele.

4c *Katika NYAKATI NYINGINE:*
Muhudumu Bwana, rehema zako ni mpya kila asubui.
Wote **Uaminifu wako ni mukubwa!**
Muhudumu Tangu mapambazuko hata mangaribi
Wote **Jina la Bwana lisifiwe.**

5 *Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine. Kwa mufano....*
Siku ya Mungu katika KUJA na KUFUNGA:
KUJENI (Venite) p 18
Siku ya Mungu katika ONYESHO:
Wimbo wa SIMIONI (Nunc Dimmitis) p 25
Siku ya Mungu katika PASAKA:
Wimbo wa UFUFUKO p 26

Siku ya kwanza: **KUJENI** (Venite) p 18
Siku ya pili: **Wimbo wa MARIA** (Magnificat) p 22
Siku ya tatu: **MUMUSIFU** (Benedicite) p 21
Siku ya ine: **Wimbo wa UFUFUKO** p 26
Siku ya tano: **Wimbo wa ROHO MUTAKATIFU** p 25
Siku ya sita: **MUBARIKI** (Te Deum) p 19

6† *Muhudumu aseme:*

Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu. Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atatuondolea zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote. *1 Yoane 1:8-9*

7 *Muhudumu aseme:*
Tukiri zambi zetu kwa Mungu Mwenyezi.
Wote wapige magoti na kusema

Mungu Mwenyezi,
Baba yetu ya mbinguni,
tumekosea wewe,
na tumekosea jirani zetu,
kwa mawazo yetu,
na kwa maneno yetu,
na kwa matendo yetu,
na kwa maovu tuliyoyatenda,
na kwa mema tusiyoyatenda,
kosa letu wenyewe.
Sisi tunatubu kabisa.
Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo,
utusamehe yote yaliyopita;
utuwezeshe tangu leo kukutumikia,
katika upya wa uzima.
Kwa utukufu wa Jina lako. Amina.

— — — — □ — — — —

8a *Kasisi au Askofu asimame na aseme:*

Mungu Mwenyezi,
mwenye kusamehe wote wanaotubu kwa kweli,
a*wa*rehemu, a*wa*samehe na a*wa*okoe
kwa zambi ze*nu* zote,
a*wa*sibitishe‡ na a*wa*pe nguvu kwa wema wote,
na a*wa*linde katika uzima wa milele,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

- - - - - - - - - - - - *AU*- - - - - - - - - - - -

8b *Muhudumu au mutu mwengine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.*

Ee Mungu, mwenye rehema, tunakusihi,
utupe sisi, watu wako waaminifu, usamehe na salama,
ili tusafishwe zambi zetu zote,
na tukutumikie na nia tulivu;
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

9† *Zaburi ya Siku isomwe au iimbwe.*
Kila Zaburi itamalizika na:

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana,
na kwa Roho Mutakatifu:
kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa,
hata milele na milele. Amina.

10† *Kuketi.*
Kipande kinachotoka AGANO LA KALE kisomwe.

Musomaji aseme kwanza:
Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa...

Na kwa mwisho aseme: Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote: **Asante kwa Mungu.**

11† *Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine. Kwa mufano....*
Katika KUJA na KUFUNGA:
Wimbo wa ZEKARIA (Benedictus) p 28
Katika KUZALIWA na ONYESHO:
UTUKUFU (Gloria) p 22
Katika PASAKA: **MUFURAHI** (Jubilate) p 20
Katika KUPANDA na PENTEKOTE:
Wimbo wa ROHO MUTAKATIFU p 25

12 *Kuketi. Kipande kinachotoka INJILI au sehemu nyingine ya AGANO JIPYA kisomwe.*
Musomaji aseme kwanza:
Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa...

Na kwa mwisho aseme: Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote **Asante kwa Mungu.**

13* *Matangazo.*

14* *Wimbo.*

15 KUHUBIRI

16† *Watu wasimame kuhakikisha* IMANI YA MITUME

Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi,
Muumba wa mbingu na dunia;

Na Yesu Kristo,
Mwana wake wa pekee, Bwana wetu,
aliyetwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu,
akazaliwa na Bikira Maria.
Akateswa zamani za Pontio Pilato,
akasulibiwa, akafa, akazikwa,
akashuka kuzimuni mwa wafu,
akafufuka katika wafu siku ya tatu,
akapanda mbinguni,
anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu,
Baba Mwenyezi,
ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu.

Ninamwamini Roho Mutakatifu,
Kanisa katolika‡ takatifu,
ushirika wa watakatifu,
ondoleo la zambi,
ufufuko wa mwili,
na uzima wa milele. Amina.

17 *Kupiga magoti*
Muhudumu Bwana utuhurumie.
Wote **Kristo utuhurumie.**
Muhudumu Bwana utuhurumie.

18 *Wote*
Baba yetu, uliye mbinguni,
jina lako litukuzwe,

ufalme wako uje,
mapenzi yako yatimizwe,
duniani kama mbinguni.
Utupe leo chakula chetu cha kila siku;
utusamehe makosa yetu,
kama tunavyowasamehe waliotukosea.
Usitulete katika majaribu,
lakini utuokoe katika uovu.
Kwani kwako ufalme,
uwezo na utukufu,
milele na milele, Amina.

19† *Muhudumu* Ee Bwana utuonyeshe rehema yako;
Wote **Utupe sisi wokovu wako.**
Muhudumu Ee Bwana uwabariki watawala wetu;
Wote **Utusikie kwa rehema yako tukikuomba.**
Muhudumu Uwavike haki wahudumu wako;
Wote **Uwafurahishe wachaguliwa wako.**
Muhudumu Ee Bwana uwaokoe watu wako;
Wote **Uubariki uriti wako.**
Muhudumu Ee Bwana utupe salama kwa siku zetu;
Wote **Na utukufu wako uwe popote duniani.**
Muhudumu Ee Mungu, utusafishe mioyo yetu;
Wote **Na ututegemeze na Roho yako Mutakatifu.**

20 SALA YA SIKU

21 SALA KWA SALAMA
Baba Mungu, uliye mukuu wa salama
na mupenda wa upatano,
kukujua wewe ni uzima wa milele,
kukutumikia wewe ni uhuru wa kweli.
Utulinde sisi watumishi wako
katika mashambulio yote ya adui zetu;
ili sisi tukitumainia ulinzi wako,
tusiogope nguvu ya adui wo wote;
kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

22* *Muhudumu na watu wanaweza kusema pamoja.*
SALA KWA NEEMA
Ee Bwana, Baba yetu ya mbinguni,
Mungu Mwenyezi unayeishi milele,
uliyetusaidia tuione siku hii salama;
utulinde leo kwa uwezo wako mukuu,
tusianguke katika zambi,
wala tusiingie katika hatari yo yote,
lakini matendo yetu yote yaongozwe nawe,
ili tuyatende siku zote yaliyo ya haki mbele yako,
kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

23† MAOMBI YA KANISA
Tuombee Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.
1. Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, kwa Mwana wako Yesu Kristo, umetuahidi kutusikia tukiomba kwa imani:
Tunakushukuru Baba kwa...
Tunaombea...
Kanisa duniani...
Jimbo letu, Dayosisi yetu, na Askofu wetu J...

Ee Mungu, ulipe Kanisa lako nguvu kuendelesha mbele kazi ya Kristo; ili sisi na wote wanaokiri jina lako, tushirikiane katika kweli yako, tuishi pamoja katika mapendo yako, na tuonyeshe utukufu wako duniani.

Ee Bwana kwa rehema yako.

Wote **Usikie kuomba kwetu**

2. Mungu, tunakushukuru kwa...
Tunaombea...
Mataifa yote duniani...
Mutawala wetu na Wakubwa...
Taifa letu...
Watu wote kwa kazi zao za kila siku...

Ee Mungu uwape akili Wakubwa wote wanaotutawala, zaidi Prezidenti yetu J. Tunakusihi uendeleshe taifa letu na mataifa yote kwa njia ya haki na salama; ili watu wote waheshimu mumoja kwa mwingine, na wafuate siku zote uzuri kwa watu wote.

Ee Bwana kwa rehema yako.

Wote **Usikie kuomba kwetu**

3. Mungu, tunakushukuru kwa...
Tunaombea...
Parokia yetu...
Nyumba zetu na rafiki zetu...
Wenye mahitaji yo yote...

Ee Mungu utupe sisi neema, kwa nyumba zetu na kwa rafiki zetu, na vile kwa jirani zetu zote; sisi sote tukutumikie kwa kuwatumikia, tuwapende kama Kristo anavyotupenda.

Ee Bwana kwa rehema yako.

Wote **Usikie kuomba kwetu**

4. Tunaombea wagonjwa na wanaoumwa na wanaokufiliwa, na wengine wenye magumu, na wale wasioamini Kristo...
Tumushukuru Mungu kwa wale wote wanaowasaidia...
Ee Mungu tunakusihi uwafariji na uwaponyeshe, wale wote walio na mateso ya mwili na ya akili na ya roho. Uwategemeze na uhodari na taraja katika mateso yao; na uwaletee furaha kwa wokovu wako. Na vile tunakushukuru na tunawaombea wale wanaowasaidia na wanaowatunza katika huzuni na mashaka yao.

Ee Bwana kwa rehema yako.

Wote **Usikie kuomba kwetu**

5. Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina**.

Ombi hili linaweza kusemwa kama ombi moja pasipo kugawanyika.

24* *Maombi mengine yanaweza kusemwa.*

25* *Muhudumu na watu wote‡:*

Mungu Mwenyezi uliyetupa neema wakati huu,
tushirikiane kwa kukuletea maombi yetu
kwa moyo mumoja;
umeahidi ya kwamba
watu wawili au watatu wakikusanyika
katika jina lako,
utawapa vile wanavyoomba;
uyatimize sasa, Ee Bwana, maombi ya watumishi wako kama vitakavyotufaa.

Utupe sisi kujua kweli yako katika dunia hii;
na katika dunia itakopokuja, utupe uzima wa milele.
Amina.

26† *Wimbo na kupokea sadaka.*

27 *Baraka au Neema.*

BARAKA - *Kasisi:* Tuombe

Salama ya Mungu, inayopita akili yote,
iwalinde mioyo na nia zenu,
katika hali ya kujua na kupenda Mungu,
na Mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu;

Na Baraka ya Mungu Mwenyezi,
Baba na Mwana na Roho Mutakatifu,
iwe kwenu na ikae nanyi,
milele na milele. **Amina.**

NEEMA - *Watu wote*

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo,
na mapendo ya Mungu Baba,
na ushirika wa Roho Mutakatifu,
ukae nasi sote, milele na milele. Amina.

27* *Wimbo.*